

Tanzania

**Utafiti wa Viashiria vya VVU/UKIMWI na
Malaria Tanzania 2011-12**

Matokeo Muhimu



Utafiti huu wa Viashiria vya VVU/UKIMWI na Malaria Tanzania 2011-12 (THMIS) ulifanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali - Zanzibar (OCGS-Zanzibar) kuanzia Desemba 16, 2011, hadi Mei 24, 2012. Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Zanzibar (ZAC) zilitoa idhini ya kufanyika kwa utafiti huu. Utafiti huu ulifadhiliwa na Shirika la Misaada ya Maendeleo la Watu wa Marekani (USAID), TACAIDS na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (MoHSW). ICF International ilisaidia kufanyika kwa utafiti huu kupitia mradi wa MEASURE DHS unaofadhiliwa na USAID. Mradi wa MEASURE DHS unatoa msaada wa kiufundi na fedha kwa tafiti za demografia na afya katika nchi mbalimbali duniani.

Taarifa za ziada kuhusiana na utafiti huu zinapatikana Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) P.O. Box 76987, Dar es Salaam, Tanzania (Simu: 255-22-212-2651; Nukushi: 255-22-212-2427; Tovuti: www.tacaids.go.tz) na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Makao Makuu, P.O. Box 796, Dar es Salaam, Tanzania (Simu: 255-22-212-2722/3; Nukushi 255-22-213-0852; Tovuti: www.nbs.go.tz).

Taarifa kuhusu program ya DHS zinapatikana MEASURE DHS, ICF International, 11785 Beltsville Drive, Suite 300, Calverton, MD 20705, USA (Simu: 301-572-0200; Nukushi: 301-572-0999; Barua pepe: reports@measuredhs.com; Tovuti: <http://www.measuredhs.com>.)

Kunukuu taarifa hizi:

Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), Tume ya Kudhibiti UKIMWI Zanzibar (ZAC), Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali - Zanzibar (OCGS), na ICF International. 2013. *Utafiti wa Viashiria vya VVU/UKIMWI na Malaria Tanzania 2011-12: Matokeo Muhimu*. Dar es Salaam, Tanzania: TACAIDS, ZAC, NBS, OCGS, na ICF International.

Picha katika jalada: © UNICEF Tanzania 2008/262/GiacomoPirozzi



USAID
FROM THE AMERICAN PEOPLE



President's Malaria Initiative



KUHUSU THMIS 2011-12

Utafiti wa Viashiria vya VVU/UKIMWI na Malaria Tanzania 2011-12 (THMIS) ulifanywa kwa ajili ya kukusanya taarifa mpya za kiwango cha maambukizi ya VVU mionganoni mwa watu wazima nchini Tanzania na kiwango cha malaria na upungufu wa damu mionganoni mwa watoto wenyе umri chini ya miaka mitano. THMIS 2011-12 ni utafiti wa kumi kufanyika kitaifa ukiwa ni sehemu ya mradi wa tafiti za Demografia na Afya nchini Tanzania. Ni utafiti mkubwa wa tatu kufanyika Tanzania juu ya VVU/UKIMWI.

Nani alishiriki katika Utafiti?

Sampuli wakilishi ya kitaifa ya wanawake 10,967 wenyе umri wa miaka 15-49 na wanaume 8,352 wenyе umri wa miaka 15-49 walihojiwa. Idadi hii ni mwitikio wa 96% kwa wanawake na 89% kwa wanaume. Sampuli hii inaruhusu kufanyika kwa makadirio kwa Tanzania nzima, kwa mijini na vijijini, kwa kila mojawapo ya kanda tisa, na kwa viashiria vingi, inaruhusu kufanyika makadirio kwa mikoa yote 30.

TANZANIA



Mwinuko kutoka usawa wa bahari



TAARIFA ZA KAYA NA WASHIRIKI

Kaya Nchini Tanzania

Kaya nchini Tanzania zina wastani wa watu watano. Karibu robo ya kaya zinaongozwa na wanawake. Karibu nusu ya wananchi wana umri chini ya miaka 15.

Hali ya maisha imekuwa bora kwa kiasi fulani katika maeneo ya mijini Tanzania Bara na Zanzibar kuliko maeneo ya vijijini Tanzania Bara. Karibu kaya tisa katika kila kaya kumi za mijini Tanzania Bara zinapata maji ya kunywa kutoka katika chanzo kilichoboreshwu, ukilinganisha na 47% ya kaya za vijijini Tanzania Bara. Karibu kila mahali Zanzibar kuna vyanzo vya maji ya kunywa vilivyoboreshwu. Huduma za majitaka zipo kwa kiwango kidogo nchi nzima -26% kwa kaya za mijini Bara na 7% tu ya kaya za vijijini Bara ndizo zenyenye huduma bora za majitaka. Kaya sita katika kila kaya kumi Zanzibar zinapata huduma bora ya usafi.




© UNICEF Tanzania/50200/Pudlowski

Washiriki wa Utafiti - Miaka 15-49

Asilimia kumi na nane ya wanawake wenye umri wa miaka 15-49 na 9% ya wanaume wenye umri wa miaka 15-49 hawana elimu. Zaidi ya nusu ya wanawake na wanaume wamehitimu elimu ya msingi. 1% tu ya wanawake na 2% ya wanaume wamehitimu elimu ya sekondari au zaidi.

Wanaume wana uwezekano mkubwa wa kupata habari kupitia vyombo vya habari kuliko wanawake. Zaidi ya 40% ya wanawake hawakuwa na uwezekano wa kupata taarifa kupitia vyombo vya habari angalau kila wiki ukilinganisha na 23% tu ya wanaume. Redio ni njia inayotumiwa na wengi kupata taarifa: 74% ya wanaume na 49% ya wanawake wanasikiliza redio kila wiki.




Asilimia 15 ya kaya Tanzania zina umeme, idadi imeongezeka kidogo kutoka 12% ya mwaka 2007-08. Tanzania Bara, kuna tofauti kubwa katika upatikanaji wa umeme baina ya kaya za mijini na za vijijini (46% dhidi ya 4%). Kwa upande wa Zanzibar, 41% ya kaya zina umeme.

Zaidi ya 60% ya kaya nchini Tanzania zina redio, wakati 15% tu ndizo zenyenye TV. Asilimia sitini na moja ya kaya zina simu ya mkononi. Karibu kaya moja katika kila kaya tano zina akaunti benki. Karibu nusu ya kaya zina baiskeli wakati 2% tu ya kaya zina gari au lori.

Elimu

Asilimia ya wanawake na wanaume miaka 15-49 kwa kiwango cha juu cha elimu walichonacho.



UFAHAMU NA MITAZAMO KUHUSU VVU/UKIMWI

Ufahamu wa Njia za Kujikinga na VVU

Kila mtu anafahamu kuhusu VVU: Karibu washiriki wote wamesikia kuhusu UKIMWI. Zaidi ya 60% ya wanawake na 71% ya wanaume wenye miaka 15-49 wanafahamu kwamba unaweza kujikinga dhidi ya maambukizi ya VVU kwa kutumia kondom na kwa kuwa na mpenzi mmoja tu mwaminifu asiye na maambukizi. Wanaume wana ufahamu mkubwa zaidi wa njia mbalimbali za kujikinga dhidi ya maambukizi ya VVU kuliko wanawake. Ufahamu wa njia za kujikinga dhidi ya maambukizi ya VVU ni mkubwa zaidi mionganoni mwa wanawake na wanaume wa mijini na ni mkubwa zaidi kwa wale wanaotoka katika kaya tajiri.


Ufahamu Kuhusu Maambukizi ya VVU Kutoka kwa Mama Kwenda kwa Mtoto (PMTCT)

Wakati 85% ya wanawake na 79% ya wanaume wanafahamu kwamba mtoto anaweza kuambukizwa VVU kwa kunyonyeshwa, theluthi-mbili tu ya wanawake na wanaume ndio wanaofahamu kwamba hatari ya mama kumwambukiza mtoto inaweza kupungua ikiwa mama atatumia dawa maalumu wakati wa ujauzito. Karibu theluthi-mbili (64%) ya wanawake na zaidi ya nusu ya wanaume (55%) wanafahamu mambo yote hayo mawili kuhusu kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Ufahamu wa wanawake na wanaume kwamba hatari ya mama kumwambukiza mtoto inapungua ikiwa mama atatumia dawa maalum wakati wa ujauzito umeongezeka tangu utafiti wa THIMIS wa mwaka 2007-08.

Mwenendo wa Ufahamu wa Maambukizi ya VVU ya Mama kwa Mtoto

Asilimia ya wanawake na wanaume miaka 15-49 wanaofahamu kwamba:




Mitazamo dhidi ya watu wanaoishi na VVU/UKIMWI

Unyanyapaa na ubaguzi unaohusiana na VVU/UKIMWI bado vimeenea sana mionganoni mwa watu wazima nchini Tanzania. Ingawa wanawake walio wengi (93%) na wanaume (96%) wanasema kwamba wako tayari kumhudumia mwanafamilia mwenye UKIMWI katika nyumba zao wenye, 41% tu ya wanawake na 57% ya wanaume wanasema kwamba wasingependa iwe siri ikiwa mwanafamilia ana VVU. Zaidi ya hayo robo tu ya wanawake na 40% ya wanaume wanaonyesha mitazamo chanya dhidi ya watu waishio na VVU/UKIMWI kwa viashiria vyote vinne.

Wanawake na wanaume Zanzibar wanaonyesha kiwango kidogo cha unyanyapaa unaohusiana na VVU/UKIMWI ukilinganisha na wa Tanzania Bara. Asilimia arobaini na tatu ya wanawake na 55% ya wanaume Zanzibar wanaonyesha mitazamo ya kuwakubali watu waishio na VVU/UKIMWI kwa viashiria vyote vinne ukilinganisha na 25% ya wanawake na 40% ya wanaume Tanzania Bara.

Mitazamo Dhidi ya Watu Waishio na VVU/UKIMWI

Asilimia ya wanawake na wanaume miaka 15-49 ambao:




© UNICEF Tanzania/11-2321/Pudlowski

TABIA ZA WATU KUHUSIANA NA NGONO

Wenzi Zaidi ya Mmoja kwa Mikoa: Wanawake

Asilimia ya wanawake miaka 15-49 waliokuwa wamejamiiiana na wenzi 2+ miezi 12 kabla ya utafiti



Asilimia nne ya wanawake Tanzania wenyewe miaka 15-49 waliripoti kuwa na wenzi wawili au zaidi waliojamiiiana nao miezi 12 kabla ya utafiti. Suala la kuwa na wenzi wengi linatofautiana kati ya kiwango kidogo kabisa cha <1% Mikoa ya Katavi, Iringa, Pemba na Unguja na kiwango cha juu 9% katika mikoa ya Mara na Mtwara.


Asilimia tisa ya wanaume waliripoti kulipia ngono miezi 12 kabla ya utafiti. Zaidi ya nusu (53%) ya wanaume waliojihusisha na ngono kwa kulipia miezi 12 iliyopita walitumia kondom mara ya mwisho walipolipia ngono.

Matumizi ya Kondom

Asilimia ishirini na saba ya wanawake na wanaume waliokuwa na wenzi zaidi ya mmoja miezi 12 iliyopita waliripoti kutumia kondom mara ya mwisho walipojamiiiana. Matumizi ya kondom mionganoni mwa watu wenyewe wenzi zaidi ya mmoja yanaongezeka sambamba na ongezeko la kiwango cha elimu.

Matumizi ya Kondom Mionganoni mwa Walioripoti Kuwa na Wenzi Wengi kwa Viwango Vyao vya Elimu


Mionganoni mwa wanawake na wanaume miaka 15-49 waliokuwa wamejamiiiana na wenzi 2+ miezi 12 kabla ya utafiti, asilimia ya waliosema walitumia kondom mara ya mwisho walipojamiiiana.



*Takwimu katika paradesi zinatokana na matukio 25-49.

Wenzi Zaidi ya Mmoja kwa Mikoa: Wanaume

Asilimia ya wanaume miaka 15-49 waliokuwa wamejamiiiana na wenzi 2+ miezi 12 kabla ya utafiti



Uwiano wa wanaume wenyewe miaka 15-49 ambao walikuwa wamejamiiiana na wenzi wawili au zaidi miezi 12 iliyopita ni zaidi ya mara tano ya uwiano wa wanawake (21% dhidi ya 4%). Mionganoni mwa wanaume, kuwa na wenzi wengi ni jambo ambalo lipo zaidi katika mikoa ya Ruvuma (34%) na Geita (31%).



© UNICEF Tanzania/10/Gomi

UPIMAJI WA VVU


Wanawake na wanaume tisa katika kila kumi wanafahamu mahali pa kupata huduma ya upimaji wa VVU. Upimaji wa VVU nchini Tanzania umekuwa ukiongezeka siku hadi siku. Upimaji wa VVU na upokeaji wa majibu umeongezeka mionganoni mwa wanawake wenye miaka 15-49 kutoka 37% mwaka 2007-08 hadi 62%. Vivyo hivyo, kupima VVU na kupokea majibu kumeongezeka karibu mara mbili mionganoni mwa wanaume kutoka 27% mwaka 2007-08 hadi 47%. Hata hivyo, theluthi-moja ya wanawake na nusu ya wanaume hawajawahi kupima VVU.

Upimaji wa VVU mionganoni mwa wanawake na wanaume ni mkubwa zaidi mijini kuliko vijijini. Wanawake na wanaume walioolewa/waliooa au wanaoishi na wenzi wana uwezekano mkubwa zaidi wa kuwa wamewahi kupima na kupokea majibu kuliko wale ambao wametalikiana, wametengana, wajane, au wale ambao hawakuwahi kuolewa. Upimaji wa VVU unaongezeka sambamba na ongezeko la kiwango cha elimu kwa wanaume; 54% ya wanaume wenye elimu ya sekondari au zaidi wamewahi kupima VVU na kupokea majibu ukilinganisha na 32% ya wanaume ambao hawana elimu.

Wanawake watatu katika kila wanawake 10 na zaidi ya 25% ya wanaume wamewahi kupima VVU na kupokea majibu miezi 12 kabla ya utafiti.

Upimaji wa VVU kwa Mikoa: Wanawake

Asilimia ya wanawake miaka 15-49 waliowahi kupima VVU na kupokea majibu




Takriban theluthi-mbili ya wanawake Tanzania wenye miaka 15-49 wamewahi kupima na kupokea majibu yao. Upimaji wa VVU ni mkubwa zaidi katika mikoa ya Njombe na Lindi (74% kila moja) na ni wa chini zaidi katika mikoa ya Katavi na Rukwa, ambako chini ya nusu ya wanawake wamewahi kupima VVU na kupokea majibu yao.

Mwenendo wa Upimaji wa VVU

Asilimia ya wanawake na wanaume miaka 15-49 waliowahi kupima VVU na kupokea majibu


■ 2007-08 THMIS ■ 2010 TDHS ■ 2011-12 THMIS



© UNICEF Tanzania/92/Pirozzi

Upimaji wa VVU kwa Mikoa: Wanaume

Asilimia ya wanaume miaka 15-49 waliowahi kupima VVU na kupokea majibu




Takriban nusu ya wanaume wenye miaka 15-49 wamewahi kupima VVU na kupokea majibu yao. Upimaji wa VVU unatofautiana kutoka kiwango cha juu cha 65% mkoani Njombe hadi kiwango cha chini cha 29% mkoani Arusha. Upimaji wa VVU ni mkubwa mionganoni mwa wanaume wenye kiwango bora cha elimu na wanaotoka katika kaya tajiri.

VIJANA NA VVU

Umri Wakati wa Kujamiiiana kwa Mara ya Kwanza

Asilimia tisa ya wasichana na 10% ya wavulana wenyi miaka 15-24 waliripoti kujamiiiana kwa mara ya kwanza kabla ya kutimiza miaka 15. Mionganii mwa wenyi miaka 18-24, 50% ya wasichana na 43% ya wavulana waliripoti kufanya ngono wakiwa na miaka 18.

Umri Wakati wa Kuanza Kujamiiiana



Nongo Kabla ya Ndoa

Karibu theluthi-moja ya wasichana ambao hawajawahi kuolewa na 42% ya wavulana ambao hawajawahi kuoa walikuwa wamejamiiiana miezi 12 kabla ya utafiti. Matumizi ya kondom mara ya mwisho ya kujamiiiana yalikuwa ni karibu kwa kiwango sawa kwa makundi yote mawili (58% na 59%) na yaliongezeka kutoka 49% mwaka 2007-08. Wasichana ambao hawajawahi kuolewa wana uwezekano mkubwa wa kuripoti kwamba hawajawahi kujamiiiana (59%) kuliko wavulana ambao hawajawahi kuoa (48%).

Ushauri Nasaha na Upimaji wa VVU


Mionganii mwa vijana wenyi miaka 15-24, karibu nusu ya wasichana na theluthi-moja ya wavulana wamewahi kupima VVU na kupokea majibu yao. Wasichana na wavulana wenyi miaka 20-24 wana uwezekano mkubwa wa kuwa wamewahi kupima VVU na kupokea majibu yao kuliko wasichana na wavulana wadogo zaidi, miaka 15-19.

TOHARA KWA WANAUUME

Karibu robo-tatu (72%) ya wanaume Tanzania wenyi miaka 15-49 wameripoti kwamba wametahiriwa. Tohara kwa wanaume inafanyika zaidi mijini kuliko vijiji (94% dhidi ya 64%). Zaidi ya nusu ya mikoa Tanzania Bara ina kiwango kinachofikia 50% au zaidi cha tohara kwa wanaume. Tohara kwa wanaume ni ya kiwango cha chini zaidi katika mikoa ya Rukwa (28%), Simiyu (30%) na Shinyanga (32%). Kinyume chake, karibu wanaume wote katika mikoa ya Zanzibar, Dar es Salaam, Mtwara, Tanga, Lindi, na Pwani wametahiriwa.

Tohara kwa Wanaume kwa Mikoa

Asilimia ya wanaume miaka 15-49 waliotahiriwa



© UNICEF Tanzania/03/Gomi

KIWANGO CHA MAAMBUKIZI YA VVU/UKIMWI


Taarifa za kiwango cha maambukizi ya VVU/UKIMWI zilipatikana kutokana na sampuli za damu zilizotolewa kwa hiyari na wanawake na wanaume waliohojiwa katika THMIS 2011-12. Kati ya wanawake na wanaume 20,811 wenye miaka 15-49 walioshiriki katika utafiti, 90% ya wanawake na 79% ya wanaume walitoa sampuli za damu kwa ajili ya upimaji wa VVU.

Kwa ujumla, 5.1% ya Watanzania wenye miaka 15-49 wana maambukizi ya VVU. Kiwango cha maambukizi ya VVU ni kikubwa miongoni mwa wanawake (6.2%) kuliko kwa wanaume (3.8%). Kiwango cha maambukizi ya VVU ni kikubwa zaidi maeneo ya mijini kwa wanawake na wanaume kuliko maeneo ya vijijini.

Maambukizi ya VVU kwa Makazi

■ Mijini ■ Vijiijini ■ Tanzania kwa ujumla

*Asilimia ya wanawake na wanaume miaka 15-49
wenye VVU*




Kiwango cha maambukizi ya VVU ni kikubwa zaidi miongoni mwa watu waishio katika kaya tajiri zaidi. Katika mikoa, kiwango cha maambukizi ya VVU kinatofautiana kutoka chini ya 1% katika Mkoa wa Pemba na 1.2% katika Mkoa wa Unguja hadi kiwango cha juu ambacho ni 14.8% katika Mkoa wa Njombe.

Mwenendo wa Maambukizi ya VVU Tanzania (Bara na Zanzibar)

■ 2007-08 THMIS ■ 2011-12 THMIS


Asilimia ya wenyewe maambukizi ya VVU



Kwa kulinganisha kiwango cha maambukizi ya VVU katika THMIS 2007-08 na kile cha THMIS 2011-12, inaonyesha kwamba kiwango cha maambukizi kimepungua kidogo kutoka 5.7% hadi 5.1% miongoni mwa watu wazima wenye miaka 15-49. Vivyo hivyo, kiwango cha maambukizi ya VVU kimepungua miongoni mwa wanawake, kutoka 6.6% hadi 6.2%, na miongoni mwa wanaume, kutoka 4.6% hadi 3.8%. Viwango hivi vya kupungua kwa maambukizi sio vikubwa kiasi cha kuwa muhimu kitakwimu.

Maambukizi ya VVU kwa Mikoa

*Asilimia ya wanawake na wanaume
miaka 15-49 wenye maambukizi ya VVU*




© UNICEF Tanzania/711/Pirozzi

Mwenendo wa Maambukizi ya VVU Tanzania Bara (Haihusishi Zanzibar)

■ 2003-04 THIS ■ 2007-08 THMIS ■ 2011-12 THMIS

Asilimia ya wenyewe maambukizi ya VVU



Tanzania Bara, kiwango cha maambukizi ya VVU miongoni mwa wanawake na wanaume wenye miaka 15-49 kimepungua kutoka 7.0% katika THIS 2003-04 hadi 5.3% katika THMIS 2011-12. Kupungua kwa kiwango cha maambukizi ya VVU kwa ujumla wake kati ya 2003-04 na 2011-12 ni cha kuridhisha kitakwimu. Zaidi ya hayo, kupungua kwa kiwango cha maambukizi miongoni mwa wanaume ni cha kuaminika kitakwimu (6.3% dhidi ya 3.9%).

KIWANGO CHA MAAMBUKIZI YA VVU


Kiwango cha Maambukizi ya VVU kwa Hali ya Ndoa

Kiwango cha maambukizi ya VVU ni kikubwa zaidi miongoni mwa wanawake na wanaume wajane. Kiwango cha maambukizi ya VVU pia ni kikubwa miongoni mwa wanawake na wanaume walitalikiana na waliotengana na wenzi wao. Wanawake na wanaume ambao hawajawahi kuolewa wana uwezekano mdogo zaidi wa kuwa na maambukizi ya VVU.

Maambukizi ya VVU kwa Hali ya Ndoa

■ Wanawake 15-49 ■ Wanaume 15-49

Asilimia ya wenyewe maambukizi ya VVU




*Takwimu katika paradesi zinatokana na matukio 25-49.

Kiwango cha Maambukizi ya VVU kwa Umri

Miongoni mwa wanawake na wanaume, kiwango cha maambukizi ya VVU kinaongezeka sambamba na kuongezeka kwa umri. Wanawake wengi zaidi wana maambukizi ya VVU ukilinganisha na wanaume katika kila rika.

Maambukizi ya VVU kwa Umri




Maambukizi ya VVU kwa Vijana

Kwa ujumla, 2.0% ya wasichana na wavulana wenyewe miaka 15-24 wana maambukizi ya VVU, idadi ambayo ni karibu sawa na ile ya mwaka 2007-08. Kiwango cha maambukizi ya VVU miongoni mwa wasichana ni cha juu kuliko kwa wavulana, hususan kwa vijana wa miaka 23-24 ambapo wasichana wana uwezekano mkubwa zaidi ya mara mbili wa kuwa na maambukizi kuliko wavulana (6.6% dhidi ya 2.8%). Mkoja wa Njombe una kiwango cha juu zaidi cha maambukizi ya VVU miongoni mwa vijana 5.1%.

Maambukizi ya VVU Miongoni mwa Vijana


■ Wanawake ■ Waume
Asilimia ya wasichana na wavulana miaka 15-24 wenyewe maambukizi ya VVU



Maambukizi ya VVU na Tohara kwa Wanaume

Wanaume walitahiriwa wana uwezekano mdogo wa kuwa na maambukizi ya VVU kuliko wanaume ambao hawajatahiriwa (3.3% dhidi ya 5.2%). Miongoni mwa wanaume walitahiriwa, kiwango cha maambukizi ya VVU ni kikubwa zaidi Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Magharibi (7.0%) na ni cha chini zaidi Kanda ya Kusini (1.4%). Kiwango cha maambukizi kwa wanaume wasiotahiriwa kinaongezeka sambamba na umri hadi kufikia kilele katika miaka 35-39 (11.3%).

VVU kwa Tohara kwa Umri




KUDHIBITI NA KUTIBU MALARIA

Umiliki na Matumizi ya Chandarua

Asilimia 91 ya kaya zote nchini Tanzania zinamiliki angalau chandarua kimoja kilichowekwa dawa, na 90% zinamiliki angalau chandarua kimoja kilichowekwa dawa ya muda mrefu. Hata hivyo, 56% tu ya kaya ndizo zenye idadi ya kutosha ya vyandarua vilivyowekwa dawa kwa ajili ya wanakaya wote, kwa makadirio ya chandarua kimoja kwa watu wawili. Miongoni mwa wanakaya, 75% ya watu katika kaya wanatumia chandarua chenye dawa, wakati 68% walilala katika chandarua chenye dawa usiku wa kuamkia siku ya utafiti.

Umiliki, Upatikanaji na Utumiaji wa Chandarua Chenye Dawa




*Kwa makadirio ya chandarua kimoja kwa watu 2

Mwenendo wa Matumizi ya Chandarua Chenye Dawa

Watoto na wanawake wajawazito ni makundi ambayo yako katika hatari kubwa ya kupata malaria. Mwaka 2011-12, 72% ya watoto chini ya miaka mitano na 75% ya wajawazito walilala katika chandarua chenye dawa usiku wa kuamkia siku ya utafiti. Matumizi ya chandarua chenye dawa kwa wanakaya, watoto chini ya miaka mitano, na wanawake wajawazito yameongezeka kiasi tangu 2004-05.

Mwenendo wa Matumizi ya Chandarua Chenye Dawa

Asilimia ya walilala katika chandarua chenye dawa usiku wa kuamkia siku ya utafiti



Tiba ya Kinga ya Malaria kwa Wajawazito

Malaria wakati wa ujauzito inachangia watoto kuzaliwa wakiwa na uzito mdogo, vifo ya watoto wachanga na matatizo mengine. Ili kuzuia malaria, wajawazito wanapaswa kupewa dozi mbili au zaidi za SP/Fansidar wanapokwenda kliniki. Karibu theluthimoga (32%) ya wajawazito walipata tiba hii ya kinga ya malaria (IPTp) walipokwenda kliniki.

Malaria kwa Watoto

Katika wiki mbili kabla ya utafiti, mtoto mmoja katika kila watoto watano wenye umri chini ya miaka mitano alikuwa amepata homa, dalili ya kuu ya malaria. Zaidi ya robo-tatu (77%) ya watoto waliokuwa wamepata homa walipelekwa kituo cha huduma za afya kwa matibabu, wakati 25% ndio walifanyiwa kipimo cha damu cha malaria.

Wakati utafiti unafanyika, Dawa Mseto ya Malaria (ACT) ndio ambayo ilikuwa imependekewza kutumika kutibu malaria kwa watoto. Zaidi ya nusu (54%) ya watoto waliokuwa wamepata homa walipatiwa dawa ya malaria. Miongoni mwa watoto hawa, 61% walipatiwa Dawa Mseto ya Malaria (ACT).

Upuliziaji wa Dawa Ndani ya Nyumba

Upuliziaji wa dawa ndani ya nyumba unafanyika zaidi katika baadhi tu ya mikoa nchini Tanzania. 14% tu ya kaya nchini Tanzania ndizo zilizokuwa zimepuliza dawa ya kuangamiza wadudu ndani ya nyumba mwaka mmoja kabla ya utafiti. Upuliziaji wa dawa ulikuwa zaidi katika mikoa ya Kagera na Zanzibar, ambapo Kagera 92% na Zanzibar 87% ya kaya zilikuwa zimepuliziwa.



UPUNGUFU WA DAMU NA MALARIA

Watoto wote wenyewe miezi 6-59 wanaoishi katika kaya zilizoshiriki katika utafiti walistahili kupima kiwango cha upungufu wa damu na malaria. Upimaji wa kiwango cha upungufu wa damu ulifanywa kwa kutumia mashine ya HemoCue. Upimaji wa malaria ulifanywa kwa kutumia kipimo cha papo kwa hapo (RDT) pamoja na kipimo cha kawaida cha kutumia darubini. Kati ya watoto 8,119 waliostahili kupima, 95% walitoa damu kwa ajili ya upimaji wa kiwango cha upungufu wa damu, 94% kwa kipimo cha papo kwa hapo, na 92% kwa kipimo cha kutumia darubini. Ripoti hii inatoa makadirio ya kiwango cha malaria kutohaka na matokeo ya kipimo cha papo kwa hapo (RDT) cha damu cha malaria pekee.


Kiwango cha Upungufu wa Damu

Upungufu wa damu ni dalili kubwa ya malaria kwa watoto. Nchini Tanzania, 6% ya watoto wenyewe miezi 6-59 wana upungufu wa damu kiasi hadi wa kiwango kikubwa. Upungufu wa damu wa wastani hadi ule wa kiwango kikubwa unapungua kadri umri unavyoongezeka.

Tatizo la upungufu wa damu kwa watoto ni kubwa zaidi katika mikoa ya Arusha (16%) na Lindi (12%) na ni dogo zaidi Kilimanjaro ambako chini ya 1% ya watoto wenyewe miezi 6-59 wana upungufu wa damu.

Upungufu wa Wastani wa Damu Hadi Upungufu Mkubwa wa Damu Miiongoni mwa Watoto

Asilimia ya watoto miezi 6-59 wenyewe upungufu wa damu wa wastani hadi upungufu mkubwa (haemoglobin <8.0g/dl)




© 2007 Bonnie Gillespie, Courtesy of Photostock

Malaria

Nchini Tanzania, 9% ya watoto wenyewe miezi 6-59 walikutwa na malaria walipofanyiwa kipimo cha damu cha papo kwa hapo (RDT). Kiwango cha malaria kinaongezeka sambamba na umri. Kiwango cha malaria ni kikubwa zaidi maeneo ya vijiji (10%) kuliko maeneo ya mijini (3%).

Malaria kwa Watoto

Asilimia ya watoto miezi 6-59 waliopimwa na kukutwa na malaria kwa kipimo cha damu cha papo kwa hapo (RDT)




Umri kwa miezi

Viwango vya malaria vinatofautiana sana baina ya mikoa. Kiwango cha malaria ni kikubwa zaidi katika mikoa ya Geita (32%), Kigoma (26%), na Lindi (26%). Kiwango cha malaria ni kikubwa zaidi Tanzania Bara (10%) ukilinganisha na Zanzibar (<1%).

Malaria kwa Watoto kwa Mikoa

Asilimia ya watoto miezi 6-59 waliopimwa na kukutwa na malaria kwa kipimo cha papo kwa hapo (RDT)



UFAHAMU WA MALARIA NA UPATIKANAJI WA TAARIFA

Kiwango cha Ufahamu wa Malaria

Asilimia sabini na nane ya wanawake na 70% ya wanaume waliripoti kwamba homa ni dalili ya malaria kwa mtoto mdogo.

Karibu kila mtu anafahamu kwamba kuna uwezekano wa kujikinga dhidi ya malaria. Miongoni mwa wanaume na wanawake wanaofahamu kwamba malaria inaweza kudhibitiwa, 98% walitaja kulala katika chandaria kama njia ya kujikinga dhidi ya malaria. Hata hivyo, 4% tu ya wanawake na 2% ya wanaume ndio walioataja tiba ya kinga ya malaria kwa wajawazito (IPTp) kama njia ya kujikinga dhidi ya malaria.

Upatikanaji wa Taarifa Kupitia Vyombo vya Habari

Asilimia themanini na nne ya wanawake na 93% ya wanaume wamewahi kusikia ujumbe wa '*Malaria Haikubaliki*' au '*Maliza Malaria*' katika mwaka mmoja uliopita. Redio ilikuwa ni chombo ambacho watu wengi wamepata ujumbe huo (84% ya wanawake na 91% ya wanaume).



© UNICEF Tanzania 2008/278/Pirozzi



© UNICEF Tanzania 2008/525/Pirozzi

Programu ya HatiPunguzo

Miongoni mwa wanawake na wanaume Tanzania Bara, zaidi ya 8 katika 10 wamesikia kuhusu *HatiPunguzo*, vocha inayomwezesha mama mjamzito na mtoto mchanga kupata chandaria chenye dawa. Wanawake wengi walisikia kuhusu *HatiPunguzo* katika kituo cha huduma za afya (74%), ikifuatiwa na redio (46%). Kwa wanaume, chanzo cha taarifa kilichotajwa na wengi ni redio (74%), ikifuatiwa na kituo cha huduma za afya (48%).

Karibu theluthi-mbili ya wanawake Tanzania Bara waliojfingua mtoto hai miaka mitano iliyopita waliopata huduma za kliniki ya wajawazito walipatiwa vocha ya *HatiPunguzo*. Miongoni mwa wanawake walipatiwa vocha, zaidi ya nusu walipata vocha hiyo walipohudhuria kliniki kwa mara ya kwanza.

VIASHIRIA MUHIMU

Makazi

Ufahamu Kuhusu VVU/UKIMWI	Jumla	Mijini	Vijiji
Wanawake wenye miaka 15-49 wanaofahamu kwamba hatari ya maambukizi ya VVU inaweza kupunguzwa kwa kutumia kondom na kuwa na mwenzi mmoja tu mwaminifu asiyekuwa na maambukizi (%)	63	75	59
Wanaume miaka 15-49 wanaofahamu kwamba hatari ya maambukizi ya VVU inaweza kupunguzwa kwa kutumia kondom na kuwa na mwenzi mmoja tu mwaminifu asiyekuwa na maambukizi (%)	71	74	69
Wanawake miaka 15-49 wanaofahamu kwamba mama anaweza kumwambukiza mtoto VVU anapomnyonyesha na kwamba hatari ya mama kumwambukiza mtoto (MTCT) inapungua ikiwa mama atatumia dawa maalum wakati wa ujauzito (%)	64	78	59
Wanaume miaka 15-49 wanaofahamu kwamba mama anaweza kumwambukiza mtoto VVU anapomnyonyesha na kwamba hatari ya mama kumwambukiza mtoto (MTCT) inapungua ikiwa mama atatumia dawa maalum wakati wa ujauzito (%)	55	63	52
Wanawake miaka 15-49 wenye ufahamu wa kina kuhusu UKIMWI ¹ (%)	42	55	37
Wanaume miaka 15-49 wenye ufahamu wa kina kuhusu UKIMWI ¹ (%)	50	58	47
Wasichana miaka 15-24 wenye ufahamu wa kina kuhusu UKIMWI ¹ (%)	40	52	36
Wavulana miaka 15-24 wenye ufahamu wa kina kuhusu UKIMWI ¹ (%)	47	56	43
Tabia Kuhusiana na VVU/UKIMWI			
Wanawake miaka 15-49 waliokuwa na wenzi 2+ waliojamiaana nao miezi 12 kabla ya utafiti (%)	4	5	4
Wanaume miaka 15-49 waliokuwa na wenzi 2+ waliojamiaana nao miezi 12 kabla ya utafiti (%)	21	17	22
Wanaume miaka 15-49 ambao wametahiriwa (%)	72	94	64
Wasichana miaka 15-24 waliokuwa wamejamiiana kabla ya kutimiza miaka 15 (%)	9	7	10
Wavulana miaka 15-24 waliokuwa wamejamiiana kabla ya kutimiza miaka 15 (%)	10	7	11
Wasichana ambao hawajawahi kuolewa wenye miaka 15-24 waliokuwa wamejamiiana miezi 12 kabla ya utafiti (%)	32	39	29
Wavulana ambao hawajawahi kuo wenye miaka 15-24 waliokuwa wamejamiiana miezi 12 kabla ya utafiti (%)	42	42	42
Upimaji wa VVU			
Wanawake miaka 15-49 waliowahi kupima VVU na kupokea majibu (%)	62	70	60
Wanaume miaka 15-49 waliowahi kupima VVU na kupokea majibu (%)	47	57	44
Kiwango cha VVU			
Wanawake miaka 15-49 wenye maambukizi ya VVU (%)	6.2	8.9	5.1
Wanaume miaka 15-49 wenye maambukizi ya VVU (%)	3.8	5.2	3.4
Kuzuia na Kutibu Malaria			
Kaya zenyenye angalau chandarua kimoja kilichowekwa dawa (ITN) (%)	91	87	92
Watoto chini ya miaka mitano waliolala katika chandarua chenyeye dawa usiku wa kuamkia siku ya utafiti (%)	72	73	72
Wanawake wajawazito waliolala katika chandarua chenyeye dawa usiku wa kuamkia siku ya utafiti (%)	75	76	74
Wanawake wajawazito waliopata dozi 2+ za SP/Fansidar, angalau dozi mojawapo wakati walipokwenda kliniki (%)	32	39	30
Upungufu wa Damu na Malaria			
Kiwango cha upungufu wa damu (watoto miezi 6-59) ² (%)	6	6	5
Kiwango cha kuenea kwa malaria (watoto miezi 6-59) kwa kipimo cha damu cha papo kwa hapo (RDT) (%)	9	3	10

1-Wanafahamu kwamba matumizi sahihi na endelevu ya kondom na kuwa na mwenzi mmoja tu asiyekuwa na maambukizi kunaweza kupunguza uwezekano wa kuambukizwa VVU, wanafahamu kwamba mtu anayeonekana kuwa mwenye afya anaweza kuwa na maambukizi ya VVU, na wanafahamu kwamba VVU haviwezi kuenea kwa kuumwa na mbu au kwa njia za miujiza/uchawi.

2-Kiwango cha wastani au kiwango kikubwa cha upungufu wa damu kinatafsiriwa kwamba ni chini ya haemoglobin 8.0g/dl

Kanda									
Mashariki	Magharibi	Kusini	Nyanda za Juu Kusini	Nyanda za Juu Kusini Magh	Kati	Kaskazini	Kanda ya Ziwa	Zanzibar	
79	68	76	70	47	63	52	61	55	
75	68	82	76	83	71	71	62	39	
76	71	81	75	60	51	54	58	75	
61	57	64	73	63	44	47	47	62	
59	44	52	43	30	43	39	36	37	
57	44	56	56	64	47	51	41	30	
56	44	52	44	30	44	33	33	34	
56	42	62	54	62	42	50	36	31	
4	4	9	3	1	3	1	6	<1	
22	12	25	27	18	21	15	24	9	
96	65	>99	67	37	92	96	49	>99	
6	14	19	7	7	9	8	12	2	
11	10	20	5	12	7	9	11	<1	
43	31	45	46	22	23	23	34	6	
53	48	56	42	36	39	32	42	15	
69	66	72	70	51	61	61	59	60	
50	53	51	55	40	45	44	45	48	
7.7	5.1	5.4	10.8	9.2	3.2	4.0	5.4	1.1	
4.1	3.4	1.4	7.2	6.5	2.1	1.7	3.9	0.9	
84	95	94	94	90	93	90	94	74	
71	79	79	75	67	72	71	72	51	
75	78	81	77	59	71	71	83	36	
47	25	43	39	30	37	35	21	48	
8	6	7	5	3	4	9	5	4	
8	17	21	8	3	1	3	15	<1	

